**4th COMMUNITY OF PRACTICE FOR LEARNER-CENTRED EDUCATION**

**Dec 2011 CONFERENCE**

# UPIMAJI; KUBORESHA UPIMAJI WA MARA KWA MARA AJILI YA MAENDELEO YA UJUZI

**Na Nancy Ng'winula**

**UPIMAJI; KUBORESHA UPIMAJI WA MARA KWA MARA AJILI YA MAENDELEO YA UJUZI**

Ujuzi ni uwezo na stadi anazopata mwanafunzi baada ya kujifunza jambo fulani kwa muda maalumu. Aidha ni zao tokea, linalotegemewa kuzaliwa ama kujengeka kwa mwanafunzi baada ya kujifunza mada fulani. Mabadiliko ya mtaala ya mwaka 2005, katika shule za msingi yalilenga juu ya ujenzi wa maana kwa mwanafunzi kwa kila atakachojifunza kwa kuoanisha na mazingira anayoishi na uzoefu wa kila siku wa shuguli anazozifanya. Hivyo ujifunzaji uhusisha milango mingi ya fahamu na hatimaye ujuzi uliokusudiwa ukajengeka. Ujuzi huu huashiria kuwepo kwa stadi ndani yake zitakazomsaidia katika maisha yake ya kila siku.

Upimaji wa mara kwa mara au endelevu ni upimaji unaongozwa na mwalimu katika kupima uelewa na utendaji wa mwanafunzi kabla ya, wakati wa, na baada ya kujifunza mada au mada ndogo. Kulingana na mchakato huu wa upimaji, utamwezesha mwalimu kujua nini mwanafunzi anafahamu na nini hafahamu, hivyo mwalimu kusimama kikati kama mwezeshaji ili kuhakikisha mwanafunzi anajifunza na kukifahamu asichokijua

Katika kuhakikisha maendeleo ya ujuzi yanakuwepo, ni budi kuimarisha eneo la upimaji wa mara kwa mara kwa mwanafunzi.Mwalimu kama mwezeshaji, ana wajibu wa kujenga utamaduni wa kuwapima  wanafunzi wake mara kwa mara kupitia mazoezi mbalimbali. Mazoezi hayo yaweza kuwa kwa mtindo wa maswali, kazi mradi, kazi za vikundi, kazi za mmoja mmoja za kufanya darasani au nyumbani. Lengo kuu la upimaji huu ni kuimarisha na kuendeleza ujuzi uliojengeka au unaojengeka.

Upimaji unatakiwa uanze kufanyika kabla ya kuanza kufundisha mada, ili kujua mwanafunzi anafahamu nini juu ya kile anachoenda kujifunza. Kwa kulinganisha na mazingira halisi aliyonayo, mwalimu atauliza maswali kwa mdomo au kwa kuandika.

Mfano; Mada ya nishati ya umeme,(darasa la pili )

Swali; Nitajie vifaa ambavyo vinavyotumia umeme

Mwanafunzi atataja vifaa vyote anavyovifahamu. Hapo mwalimu ataweza kuelewa nini mwanafunzi wake anafahamu. Huu ni upimaji wa kabla ya mada kufundishwa .

Baada ya hapo mwalimu kama mwezeshaji, atawaongoza katika kujifunza mada hiyo hadi kufikiwa kwa malengo mahususi. Wakati somo linaendelea, mwalimu atatakiwa kuuliza maswali ili kupima kila hatua ya somo lake kama imeeleweka. Anaweza kuuliza maswali kupitia mbinu shirikishi atakazozitumia katika somo lake, mfano; majadiliano, kisa mafunzo, maswali na majibu na bunguabongo. Katika kuliandaa somo lake, mwalimu anatakiwa atumie vizuri kipengere cha upimaji ambapo ataandaa upimaji kulingana na kile anachokifundisha katika hatua ile. Mfano mada ya nishati ya umeme .

HATUA ZA SOMO

| Hatua za somo | Muda | Vitendo vya ufundishaji | Vitendo vya ujifunzaji | Vitendo vya upimaji |
|---|---|---|---|---|
| Utangulizi | Dk 5 | Bungua bongo<br>-Taja vitu vitumikavyo kutupatia umeme na kuelezea umeme ni kitu gani | Kubungua bongo na kujadili katika jozi kuhusu vitu vitumikavyo kutupatia umeme na umeme nini? | Je, mwanafunzi ameweza,<br>-kueleza vitu vinavyotoa umeme<br>-kueleza umeme ni nini? |

Hivyo mwalimu, ataainisha vitendo vya upimaji katika hatua zote za somo lake, na kisha kuzifuata wakati wa ufundishaji wake. Kwa kufanya hivyo atakuwa anaujenga na kuuimarisha ujuzi uliokusudiwa kwa mada husika.

Kila baada ya somo, mwalimu atatakiwa kuhitimisha kipindi kwa kuwapa maswali au kazi ya kufanya kwa kusudio la kuwapima kile walichojifunza na kufikiwa kwa malengo mahususi.Kufikiwa kwa malengo mahususi, ndiko kunakothibitishwa kujengeka kwa stadi na mabadiliko ya tabia ambayo mwanafunzi ataweza kuyaonyesha baada ya kujifunza mada. Utendaji huu ndio unaoonesha kwamba amejifunza, na ndio unaosababisha kuzaliwa kwa ujuzi. Hivyo kila mwalimu anapaswa kuwapima wanafunzi wake mara kwa mara ili kuona uelewa na utendaji wa mwanafunzi ulipofikia.

Ili kujenga, kuendeleza na kuhimarisha ujuzi uliojengeka kwa mwanafunzi kupitia mada alizokwishajifunza, mwalimu anatakiwa awe na ratiba endelevu ya kuwapima wanafunzi wake kila baada ya kumaliza mada. Aidha atakiwa awe na ratiba ya kuwapima wanafunzi wake kila wiki, mwezi na mwisho wa muhula wa masomo

Katika ngazi ya Kata, na Wilaya na hatua hata Mkoa, unaweza kufanyika mpango wa upimaji wa pamoja kila baada ya miezi miwili. Hii itasaidia sana katika kuendeleza ujuzi, na kuwafanya walimu wafundishe kwa bidii na kutoa mafunzo rekebishi kwa wanafunzi wao.

Ili kuleta maendeleo ya ujuzi uliojengeka kwa wanafunzi, ubora wa maswali uzingatiwe. Maswali yanayotumika katika upimaji yawe yenye kupima maarifa , stadi na mwelekeo ili kubaini ujuzi uliojengeka Kiakili, kimwili na hata kitabia. Hapo itamwezesha mwalimu kujitathimini na kutathimini somo lake kama kuna maendeleo ya ujuzi yanayojitokeza kwa wanafunzi wake. Hii hujidhihirisha pale mwanafunzi atakapoonyesha stadi na mabadiliko ya kitabia .

Katika kuleta maendeleo ya ujuzi uliokusudiwa, zipo changamoto zinazoathiri suala zima la upimaji. Changamoto hizi ni :

- Upungufu wa vitabu, kwa ajili ya wanafunzi kusoma na kupata maarifa na mazoezi.
- Wingi wa wanafunzi. Hali hii humuathiri mwalimu katika kutoa na kusahihisha mazoezi. Hivyo ulazimika kutoa mazoezi machache.

- Uchache wa walimu. Hali hii husababisha walimu kuwa na vipindi vingi kwa siku. Hivyo mazoezi hayatolewi mara kwa mara na pia akitoa huwa ni maswali machache.
- Walimu kutofahamu maswali bora ya kuwapima wanafunzi. Hupenda kupima maarifa zaidi kuliko stadi na mwelekeo .
- Matumizi hafifu ya mbinu shirikishi kutokana na wingi wa wanafunzi darasani.
- Mafunzo rekebishi kutofanyika , kutokana na wingi wa wanafunzi na uchache wa walimu
- Walimu kutotumia zana katika ufundishaji wao.

Katika kukabiliana na changamoto hizi, kwa lengo la kuimarisha na kuboresha upimaji hatimaye kuleta maendeleo na ujenzi wa ujuzi, yafuatao yafanyike:

- Wazazi na wafadhiri mbalimbali wasaidiwe shule kwa kunununa vitabu. Aidha wazazi waone umuhimu wa kuwanunulia watoto wao vitabu.
- Ujenzi wa madarasa uendelee kuhamasishwa katika jamii kuondosha mlundikano wa wanafunzi.
- Serikali iendelee kuongeza nafasi za mafunzo kwa walimu, ili shule ziwe na walimu wa kutosha.
- Walimu wapewe semina ya jinsi ya kutunga maswali yenye kupima nyanja za maarifa, stadi na mwelekeo.
- Walimu wahimizwe kutoa mafunzo rekebishi ili malengo mahususi yafikiwe kwa kila mwanafunzi
- Walimu watumie zana katika ufundishaji wao, kwani uhusisha milango mingi ya fahamu katika ujifunzaji wao.